

HALMASHAURI YA JIJI



Kumb. Na. MCC.S.60/12/IV/74

Tarehe 30.09.2024

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Mwanza anapenda kuwatangazia Watanzania mwenye sifa, nafasi 1 ya ajira ya Mtendaji Mkuu (CEO) wa Timu ya Pamba Jiji (FC) yenyé makao yake Jijini Mwanza.

SIFA ZA MWOMBAJI:

1. Awe na Shahada au Diploma ya Juu katika kozi ya michezo.
2. Awe na ujuzi katika kutumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza.
3. Awe na cheti cha FIFA Transfer Matching System (TMS).
4. Awe na ujuzi katika uendeshaji wa Akaunti za mitandao ya kijamii.
5. Awe na uzoefu wa zaidi ya miaka Mitatu (3) katika kazi ya Katibu Mtendaji.
6. Awe na ujuzi na utaalamu wa kutumia Kompyuta.
7. Awe na ujuzi na uelewa kuhusiana na CAF Club Licensing Regulations

MAJUKUMU:

1. Atakuwa Mtendaji Mkuu wa Timu na kiunganishi kwa wadau wa michezo, Serikali, Halmashauri na jamii kwa ujumla.
2. Kuongoza utekelezaji wa mikakati ya maendeleo ya klabu ya muda mfupi na mrefu.
3. Kuhakikisha kuwa Sajili zote zinazohusu Klabu pamoja na wachezaji zinakamilishwa kwa wakati na kwa kuzingatia taratibu zitolewazo na TFF, CAF na FIFA.
4. Kuratibu na kusimamia shughuli zote za kila siku za Klabu.
5. Kukabiliana na changamoto zote zinazoikabili Timu ya Pamba Jiji FC.
6. Kusimamia na kutunza rasilimali zote za Klabu
7. Kushauriana na Bodi ya Klabu ya Pamba Jiji juu ya uendeshaji wa klabu inapohitajika.

9. Kufanya kazi kwa karibu na Mhasibu wa Klabu ili kuhakikisha mahitaji muhimu yanapatikana kwa wakati.
10. Kuhakikisha kuwa Kamati zote katika Klabu zinafanya kazi kwa viwango vinavyohitajika
11. Kuhakikisha kuwa analinda mahusiano yaliyopo na kuanzisha mahusiano mapya yenyetija kwa Klabu.
12. Kufanya kazi nyingine atakazoelekezwa na Bodi ya Klabu

MAMBO YA KUZINGATIA:

Waombaji wote wenye sifa zilizoanishwa hapo juu wanapaswa kutuma barua za maombi:-

- i. Picha mbili za Pasporti za hivi karibuni
- ii. Wasifu (CV)
- iii. Nakala za vyeti vya kuzaliwa, elimu, pamoja taaluma.

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 15 Oktoba, 2024 saa 9:30 mchana.

BARUA ZOTE ZA MAOMBI ZITUMWE KWA:-

Mkurugenzi,

Halmashauri ya Jiji,

S.L.P 1333,

MWANZA.

Imetolewa na:

AS.
WAKILI; KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
MKURUGENZI WA JIJI
MWANZA.

MKURUGENZI WA JIJI LA MWANZA
MWANZA